**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/w8d1eq25


# Urefu wa Irabu katika Viambishi-Awali vya Vitenzi Viso-Ukomo vya Kiswahili Sanifu

**Pius Kiraka**
*University of Dodoma, Tanzania*

***Article History***
Received: 02.01.2026
Revised: 04.08.2026
Accepted: 07.08.2026
Published: 08.08.2026

**Keywords**
Irabu
Kiswahili sanifu
Viambishi
Vitenzi

***How to cite:***
Pius Kiraka (2026). Urefu wa Irabu katika Viambishi-Awali vya Vitenzi Viso-Ukomo vya Kiswahili Sanifu. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 4(1), 47-58.

Copyright © 2026

**Ikisiri**
Makala hii inawasilisha matokeo ya utafiti iliochunguza iwapo kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, kinaweza kuathiri urefu wa irabu pindi kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya Kiswahili sanifu. Utafiti huo wa kitaamuli ulitumia usampulishaji sinasibu na nasibu ili kuteua sampuli zilizotoa data za utafiti. Data zilikusanywa maktabani, katika Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka; na uwandani, katika eneo la Mji Mkongwe, Zanzibar, kwa kutumia mbinu ya usaili. Data hizo zilikuwa vidahizo vya Kiswahili sanifu vyenye uambishaji kisarufi na uambishaji nyambulishi. Vidahizo hivyo vilitamkwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu. Matamshi hayo yalirekodiwa kwenye kinasa-sauti na kuchakatwa maabarani kwa kutumia programu ya kompyuta ili kubainisha nyakaa za irabu mbalimbali zinazotokea kwenye matamshi hayo. Uchanganuzi wa data unaonyesha kuwa kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, kinaweza kuathiri urefu wa irabu za vitenzi kulingana na vipashio vinavyotokea mwanzoni mwa shina la utenda la kitenzi husika, au kulingana na sifa za kitenzi zilizorithiwa kutoka lugha ya Mame-Bantu. Mashina ya vitenzi yanayoanza kwa konsonanti yanapoambatishiwa kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, irabu zake huendelea kuwa na urefu uleule. Mashina mengi ya vitenzi vinavyoanza kwa irabu <a->, <e->, <i-> na <o-> nayo irabu zake huwa na urefu uleule yanapoambatishiwa kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->. Hata hivyo, kuna vitenzi vichache vinavyoghairi kanuni hiyo, ambapo hukubali irabu ya kiambishi hicho kuyeyushwa na kuwa kiyeyusho cha midomo, halafu irabu inayofuatia ya shina la kitenzi hurefushwa ili kufidia urefu wa irabu iliyoyeyushwa. Kwa mashina yanayoanza kwa irabu <u->, urefu wa irabu za maumbo mapya yanayozaliwa huendelea kuwa uleule yanapoambatishiwa kiambishi-awali hicho. Zaidi ya hayo, kitenzi <kuja> ndicho kitenzi pekee cha Kiswahili sanifu chenye irabu ndefu kwenye kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->. Hata maneno mengine yanayotokana na kitenzi hicho yana irabu ndefu, au konsonanti ndefu, kwenye viambishi-awali vyake, inayopakana na mzizi wa neno, kama ilivyo irabu ndefu katika kitenzi <ku:ja>. Inavyoelekea, Kiswahili sanifu hurefusha irabu au konsonanti inayotokea kabla ya mzizi wa kitenzi <ku:ja>, au kabla ya mzizi wa maneno yanayotokana na kitenzi hicho, ili kufidia silabi ya kwanza ya mzizi wa kitenzi hicho iliyokuwepo katika lugha ya Mame-Bantu.

**Utangulizi**

Lugha ya Kiswahili imethibitika kuwa na irabu fupi pamoja na irabu ndefu kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu (Ismail, 2025; Kiraka, 2025; Nandelenga, 2025; Kiraka, 2023; Ndumiwe, 2021; Kiraka, 2013; Choge, 2009; Massamba na wenzie, 2004; Kimizi, 2003; Maganga, 1991). Aidha, Kiraka (2013) anabainisha mambo yanayosababisha kutokea kwa irabu ndefu katika maneno ya Kiswahili sanifu kuwa ni: (i) irabu ndefu kutokea kwa asili tu, au kwa nasibu, (ii) kurefushwa kwa irabu fupi katika milolongo ya konsonanti na kiyeyusho au milolongo ya konsonanti halisi, (iii) kubadili lafudhi ya kutamkia baadhi ya maneno yaliyotoholewa kutoka lugha nyinginezo, au (iv) kuungana kwa irabu katika mipaka ya mofimu.

Hata hivyo, tukichunguza kwa makini baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu, tunaona dhahiri kuwepo kwa irabu zinazotamkwa kwa wakaa mrefu zisizotokana na mazingira yanayotajwa katika utafiti huo wa Kiraka (2013). Kwa mfano, lugha hii ina vitenzi ambavyo maumbo yake ya utenda yana irabu fupi katika mzizi, kama vile <s**u**ka, ny**o**a, j**u**a, t**a**ka>, lakini mizizi hiyohiyo ya vitenzi ikiambatishiwa viambishi fulani ili kuunda maneno mapya, irabu hizo fupi za mizizi hubadilika na kusikika zikiwa na wakaa mrefu, kama vile <ms**u:**si, kiny**o:**zi, uj**u:**zi, sit**a:**ki>. Kinyume chake, baadhi ya vitenzi vya lugha hii vina irabu ndefu katika mzizi wa umbo la utenda, kama vile <d**a:**ng**a:**nya, t**u:**a>, lakini vitenzi hivyo vinapoambatishiwa viambishi fulani ili kuunda maneno mapya, irabu hizo ndefu za mzizi wa neno – zote au baadhi tu – hubadilika na kusikika zikiwa na wakaa mfupi, kama vile <da:ng**a**nyana, kit**u**o>. Hali kadhalika, sababu za kubadilika kwa wakaa wa irabu hizo hazielekei kuwa zile zinazotajwa katika utafiti huo.

Kwa mantiki hiyo, utafiti ulifanywa ili kuchunguza namna michakato mbalimbali ya uambishaji kisarufi inavyoweza kuathiri nyakaa za irabu pindi viambishi vyake vinapoambatishwa kwenye mizizi au mashina ya maneno ya Kiswahili sanifu. Mchakato mmojawapo uliochunguzwa ni ule wa uambishaji kisarufi unaowezesha kuunda maumbo ya vitenzi viso-ukomo katika lugha hii. Hivyo basi, makala hii inajadili namna kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, kinavyoathiri urefu wa irabu pindi kinapoambatishwa kwenye maumbo ya utenda ya vitenzi vya Kiswahili sanifu.

**Kiunzi cha dhana**

Data za utafiti uliochimbua makala hii zilichanganuliwa kwa kuongozwa na kiunzi kinachoundwa na dhana ya *urefu*, *urefushaji* na *ufupishaji*. Kuhusu dhana ya *urefu*, Crystal (2008) anasema kuwa *urefu* ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya fonetiki kurejelea wakaa wa sauti au kitamkwa, na katika fonolojia hurejelea nyakaa za sauti na silabi pindi zinaposababisha tofauti kiisimu. Hali kadhalika, Trask (1996) anasema kuwa dhana ya *urefu* hurejelea wakaa wa kutamkwa kwa silabi, au irabu, au irabu-unganifu, ambao huchukuliwa kuwa ni sifa ya kifonolojia. Trask anaendelea kwa kusema kuwa dhana ya *urefu* ni sifa ya kifonolojia inayojitokeza katika lugha fulani inayotofautisha vipande-sauti vinavyofanana kupitia kiasi cha muda unaotumika katika kuvitamka. Mathalani, anabainisha kuwa dhana ya *urefu* hutumiwa na lugha ya Kiitaliano kutofautisha maana ya neno /nono/ 'tisa' na /no:no/ 'babu'; lugha ya Kiswidi huitumia kutofautisha maana ya neno /je:t/ 'mbuzi' na /jet:/ '-liopewa'; nayo lugha ya Kifini huitumia kutofautisha maana ya neno /kisa/ 'mchezo' na /kis:a/ 'paka'. Naye Kiraka (2013) anabainisha kuwa lugha ya Kiswahili sanifu hutumia dhana ya *urefu* kutofautisha maana za maneno, kama vile <kaka> 'ganda tupu la yai' na <ka:ka> 'ndugu wa kiume'; <meza> 'fanya kitu kumea' na <me:za> 'kifaa cha mbao'; <sita> 'tarakimu iliyo kati ya tano na saba' na <si:ta> 'acha kutenda jambo baada ya kuonyesha nia ya kutenda au baada ya kulianza'; <choma> 'ingiza kitu chenye ncha ndani ya ngozi au nyama au kitu

laini' na <cho:ma> 'unguza kwa moto'; na <tupa> 'rusha kitu kwenda mbali' na <tu:pa> 'kifaa cha chuma cha kunolea vitu vingine'.

Utafiti huu ulichunguza dhana ya *urefu* katika vipande-sauti vya irabu kwenye maneno ya Kiswahili sanifu yenye uambishaji kisarufi. Hivyo basi, dhana ya *urefu* katika irabu ilimaanisha wakaa wa kusikika kwa irabu fulani, ambayo inaweza kuwa fupi au ndefu (Massamba, 2005a).

Dhana nyingine iliyoongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ni dhana ya *urefushaji*. Kwa mujibu wa Trask (1996), *urefushaji* ni mchakato wowote ambao, kifonetiki au kifonolojia, huongeza wakaa wa kipande-sauti, nacho mara nyingi huwa ni irabu. Katika utafiti huu, dhana ya *urefushaji* ilichunguzwa katika irabu za maneno ya Kiswahili sanifu yanayohusisha michakato ya uambishaji kisarufi. Hivyo basi, dhana ya *urefushaji irabu* ilimaanisha mchakato wowote unaoongeza idadi ya mora za irabu fulani fupi katika neno la Kiswahili sanifu lenye uambishaji kisarufi au uambishaji nyambulishi. Au, kama asemavyo Massamba (2005a), *urefushaji irabu* ni mchakato wa kuifanya irabu ambayo hapo awali ilikuwa fupi kuwa ndefu.

Nayo dhana ya tatu iliyoongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ni dhana ya *ufupishaji*. Trask (1996) anasema kuwa *ufupishaji* ni mchakato wowote wa kifonolojia unaosababisha kipande-sauti kirefu kupoteza urefu wake. Mathalani, anadai, kwa nyakati mbalimbali, irabu ndefu za Kiingereza cha Kale zilifupishwa zilipotokea kabla ya milolongo fulani ya konsonanti na katika silabi ya tatu kutoka mwisho wa neno, kama vile: *gōd-spell* > *god-spell 'gospel'* ('injili'), *cēpte* > *cepte 'kept'* ('-liotunzwa'), *Hlāf-mæsse* > *Hlammæsse 'Lammas'* ('Misa ya Mikate'), *sūþerne* > *suþerne 'southern'* ('-a kusini'). Katika utafiti huu, dhana ya *ufupishaji* ilimaanisha mchakato wowote unaopunguza idadi ya mora za kipande-sauti fulani kirefu katika neno la Kiswahili sanifu kutokana na uambishaji kisarufi. Kwa vile utafiti huu ulichunguza vipande-sauti ambavyo ni irabu, dhana ya *ufupishaji irabu* ilimaanisha mchakato wowote unaoifanya irabu yenye wakaa mrefu kuwa na wakaa mfupi, hata kama irabu hiyo hutokea katika mazingira yanayoruhusu urefushaji (Massamba, 2005a).

**Methodolojia**

Utafiti huu ulikuwa wa kitaamuli. Mbinu za usampulishaji zilizotumiwa ili kupata sampuli iliyotoa data za utafiti huu ni usampulishaji sinasibu na usampulishaji nasibu. Usampulishaji sinasibu ulitumiwa ili kuteua sampuli ya matini za Kiswahili sanifu zilizotumiwa kupata maneno ya Kiswahili sanifu yenye uambishaji kisarufi. Nao usampulishaji nasibu ulitumiwa ili kuteua sampuli ya watoa taarifa waliotumiwa kupata matamshi ya maneno hayo ya lugha hii.

Data za utafiti zilikusanywa maktabani na uwandani. Maktabani, katika Chuo Kikuu cha Dodoma, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka, kutoka kwenye sampuli isiyo nasibu, iliyoundwa na matini tatu ambazo ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (BAKITA, 2017), *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (BAKIZA, 2015), na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2014). Nako uwandani, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili kutoka kwenye sampuli nasibu iliyoundwa na wazungumzaji sita wa lugha ya Kiswahili sanifu kutoka shehia ya Malindi na shehia ya Shangani, wilaya ya Mjini Unguja, eneo la Mji Mkongwe, Zanzibar.

Data zilizokusanywa maktabani, ambazo zilikuwa vidahizo vya Kiswahili sanifu vinavyoweza kuambatishiwa kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, zilipelekwa uwandani. Huko, data hizo zilitamkwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu. Matamshi hayo yalirekodiwa kwenye kinasa-sauti na kuchakatwa maabarani kwa kutumia programu ya kompyuta iitwayo *Speech Analyzer* ili kubainisha nyakaa za irabu mbalimbali zinazotokea kwenye matamshi hayo.

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/w8d1eq25


Mwishowe, data hizo chakate zilichanganuliwa kwa kuongozwa na kiunzi cha dhana ya urefu, urefushaji na ufupishaji ili kueleza matokeo ya utafiti huo.

**Matokeo ya utafiti**

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti uliochunguza iwapo kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, huathiri urefu wa irabu pindi kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya Kiswahili sanifu. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonyesha kuwa kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya lugha hii, kinaweza kuathiri urefu wa irabu za maumbo mapya ya vitenzi yanayozaliwa kwa namna kama tatu hivi. Namna hizo zimekitwa katika aina ya vipashio vinavyotokea mwanzoni mwa shina la utenda la kitenzi husika, au athari zilizorithiwa kutoka lugha ya Mame-Bantu. Vipengele vinavyofuata vinajadili kwa kina matokeo ya uchunguzi huo.

***Kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, kinavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya Kiswahili sanifu vyenye mashina yanayoanza kwa konsonanti***

Uchanganuzi wa data za utafiti huu unaonyesha kuwa, kwa kawaida, kiambishi-awali <ku-> kinapoambatishwa kwenye shina la kitenzi linaloanza kwa konsonanti ili kuunda umbo la kitenzi kiso-ukomo, irabu ya kiambishi-awali hicho, ambayo kwa kawaida ni irabu fupi, hubaki na urefu uleule. Hali kadhalika, urefu wa vipashio vya shina la kitenzi hicho nao hauelekei kuathiriwa. Jedwali 1 linafafanua.

*Jedwali 1: Kiambishi-awali kiso-ukomo kinapokabiliana na shina la kitenzi linaloanza kwa konsonanti katika Kiswahili sanifu*

| Kiambishi-awali | + | Shina la kitenzi | → | Kitenzi kiso-ukomo | | Kiambishi-awali | + | Shina la kitenzi | → | Kitenzi kiso-ukomo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| <**ku** | + | **b**abua> | → | <**kub**abua> | | <**ku** | + | **ng'**oa> | → | <**kung'**oa> |
| <**ku** | + | **ch**emka> | → | <**kuch**emka> | | <**ku** | + | **ny**unyiza> | → | <**kuny**unyiza> |
| <**ku** | + | **d**iriki> | → | <**kud**iriki> | | <**ku** | + | **p**ata> | → | <**kup**ata> |
| <**ku** | + | **dh**oofu> | → | <**kudh**oofu> | | <**ku** | + | **r**ehemu> | → | <**kur**ehemu> |
| <**ku** | + | **f**ukua> | → | <**kuf**ukua> | | <**ku** | + | **s**imama> | → | <**kus**imama> |
| <**ku** | + | **g**awa> | → | <**kug**awa> | | <**ku** | + | **sh**ona> | → | <**kush**ona> |
| <**ku** | + | **gh**ilibu> | → | <**kugh**ilibu> | | <**ku** | + | **t**ubu> | → | <**kut**ubu> |
| <**ku** | + | **h**emka> | → | <**kuh**emka> | | <**ku** | + | **th**amini> | → | <**kuth**amini> |
| <**ku** | + | **j**ua> | → | <**kuj**ua> | | <**ku** | + | **v**izia> | → | <**kuv**izia> |
| <**ku** | + | **k**osa> | → | <**kuk**osa> | | <**ku** | + | **w**eweseka> | → | <**kuw**eweseka> |
| <**ku** | + | **l**alama> | → | <**kul**alama> | | <**ku** | + | **y**oyoma> | → | <**kuy**oyoma> |
| <**ku** | + | **m**ega> | → | <**kum**ega> | | <**ku** | + | **z**uga> | → | <**kuz**uga> |
| <**ku** | + | **n**ing'inia> | → | <**kun**ing'inia> | | <**ku** | + | pi**:**ma> | → | <**ku**pi:ma> |

***Chanzo:*** *Data za uwandani (2022).*

Tunapochunguza matamshi ya mashina ya vitenzi katika Jedwali 1, kama yalivyotamkwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu, tunaona kuwa maumbo ya vipashio vyake, na wakaa wa vipashio hivyo, huendelea kubaki uleule hata pale mashina hayo yanapoambatishiwa kiambishi-awali <ku-> na kuwa vitenzi viso-ukomo. Irabu fupi huendelea kuwa fupi, nazo irabu ndefu huendelea kuwa ndefu. Ukiacha vitenzi ambavyo mashina yake yanaanza kwa konsonanti, mashina

ya vitenzi vya Kiswahili sanifu yanaweza pia kuanza kwa vipashio vya aina nyingine. Kipengele kinachofuata kinafafanua.

***Kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, kinavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya Kiswahili sanifu vyenye mashina yanayoanza kwa irabu***

Kiambishi-awali <ku-> cha kitenzi kiso-ukomo huweza pia kuambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya Kiswahili sanifu yanayoanza kwa irabu. Uambatishaji huo huwezesha irabu mbili kupakana, au, tuseme, kukabiliana, katika mipaka ya mofimu. Uchanganuzi wa data za uwandani (2022) unaonyesha kuwa irabu mbili zinapokabiliana katika mipaka ya mofimu – hususani irabu za viambishi-awali na zile za mashina ya nomino, vivumishi, na viwakilishi – kuna uwezekano wa irabu hizo kuathiriana kwa namna kadha wa kadha, kama vile kuungana na kuzaa irabu ndefu moja; au irabu moja kuyeyushwa huku irabu nyingine ikirefushwa; au kudondoshwa kwa idadi fulani ya mora za irabu fulani. Kinyume na yote hayo, hali hiyo haielekei kutokea pindi kiambishi-awali <ku-> cha kitenzi kiso-ukomo kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya Kiswahili sanifu yanayoanza kwa irabu. Jedwali 2 linadhihirisha.

*Jedwali 2: Kiambishi-awali kiso-ukomo kinapokabiliana na shina la kitenzi linaloanza kwa irabu katika Kiswahili sanifu*

| **Kiambishi-awali** | + | **Shina la kitenzi** | → | **Kitenzi kiso-ukomo** | **Kiambishi-awali** | + | **Shina la kitenzi** | → | **Kitenzi kiso-ukomo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| <ku | + | **a**jiri> | → | <ku$^{w}$**a**jiri> | <ku | + | **i:**nza> | → | <ku$^{w}$**i:**nza> |
| <ku | + | **a**lika> | → | <ku$^{w}$**a**lika> | <ku | + | **o**a> | → | <ku$^{w}$**o**a> |
| <ku | + | **a:**mbaa> | → | <ku$^{w}$**a:**mbaa> | <ku | + | **o**gopa> | → | <ku$^{w}$**o**gopa> |
| <ku | + | **a**muru> | → | <ku$^{w}$**a**muru> | <ku | + | **o:**mba> | → | <ku$^{w}$**o:**mba> |
| <ku | + | **a:**ndamana> | → | <ku$^{w}$**a:**ndamana> | <ku | + | **o:**ndoa> | → | <ku$^{w}$**o:**ndoa> |
| <ku | + | **a:**ndisi> | → | <ku$^{w}$**a:**ndisi> | <ku | + | **o:**ngeza> | → | <ku$^{w}$**o:**ngeza> |
| <ku | + | **a:**ngalia> | → | <ku$^{w}$**a:**ngalia> | <ku | + | **o:**nja> | → | <ku$^{w}$**o:**nja> |
| <ku | + | **e**lemea> | → | <ku$^{w}$**e**lemea> | <ku | + | **o**nyesha> | → | <ku$^{w}$**o**nyesha> |
| <ku | + | **e**limika> | → | <ku$^{w}$**e**limika> | <ku | + | **o**rodhesha> | → | <ku$^{w}$**o**rodhesha> |
| <ku | + | **e:**ndelea> | → | <ku$^{w}$**e:**ndelea> | <ku | + | **u**mwa> | → | <**kuu**mwa> |
| <ku | + | **e:**ngua> | → | <ku$^{w}$**e:**ngua> | <ku | + | **u**guza> | → | <**kuu**guza> |
| <ku | + | **i**dhinisha> | → | <ku$^{w}$**i**dhinisha> | <ku | + | **u:**mba> | → | <**kuu:**mba> |
| <ku | + | **i**giza> | → | <ku$^{w}$**i**giza> | <ku | + | **u:**nda> | → | <**kuu:**nda> |
| <ku | + | **i:**mba> | → | <ku$^{w}$**i:**mba> | <ku | + | **u:**nga> | → | <**kuu:**nga> |
| <ku | + | **i:**ngia> | → | <ku$^{w}$**i:**ngia> | <ku | + | **u**zulu> | → | <**kuu**zulu> |

***Chanzo:*** *Data za uwandani (2022).*

Uchunguzi wa matamshi ya wazungumzaji ya vitenzi viso-ukomo katika Jedwali 2 unaonyesha kuwa, kwa kawaida, kiambishi-awali <ku-> cha kitenzi kiso-ukomo kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya lugha hii yanayoanza kwa irabu, vipashio vya kiambishi-awali na vile vya shina la kitenzi huendelea kubaki na sifa zilezile, kama tu inavyokuwa kwa mashina ya vitenzi yanayoanza kwa konsonanti. Irabu ya kiambishi-awali haiyeyushwi, hairefushwi, wala mora zake hazidondoshwi. Hali ni hiyohiyo pia kwa irabu ya kwanza katika shina la kitenzi. Aidha, idadi ya silabi za vipashio vinavyowekwa pamoja nayo hubaki ileile.

Kwa upande mwingine, ikiwa shina la kitenzi linaanza kwa irabu <a->, <e->, <i-> au <o->, basi wazungumzaji wa Kiswahili sanifu huelekea kutengua mlolongo wa irabu mbili – irabu ya kiambishi-awali na irabu ya shina la kitenzi – kwa kuchopeka katikati yake sauti hafifu ya kiyeyusho cha midomo, <-$^{w}$->, ili kurahisisha namna ya kutamka silabi zilizopo kwenye mlolongo huo wa irabu, k.v. <k**u**$^{w}$**a**muru>. Hata hivyo, ikiwa irabu ya kwanza ya shina la kitenzi inafanana na ile ya kiambishi-awali, mlolongo wa irabu hizo mbili zinazofanana, <-uu->, hauvunjwi kwa kuchopeka sauti yoyote, bali irabu zote mbili hutamkwa kama silabi tofauti, k.v. <k**uu**guza>, <k**uu**mwa>, <k**uu**liza>.

Ingawa mashina ya vitenzi vingi vya Kiswahili sanifu vinavyoanza kwa irabu hayaelekei kubadilika maumbo yake pindi kiambishi-awali <ku-> cha kitenzi kiso-ukomo kinapoambatishwa mwanzoni mwa mashina hayo, kunaelekea kuwa na vitenzi vichache katika lugha hii vinavyoghairi utaratibu huo. Jedwali 3 linaonyesha hivyo.

*Jedwali 3: Vitenzi vinavyobadilika maumbo pale kiambishi-awali kiso-ukomo kinapokabiliana na shina la kitenzi linaloanza kwa irabu katika Kiswahili sanifu*

| Kiambishi-awali | + | Shina la kitenzi | → | Kitenzi kiso-ukomo |
|---|---|---|---|---|
| <k**u** | + | **e**nda> | → | <k**we:**nda> |
| <k**u** | + | **i**sha> | → | <k**wi:**sha> |

***Chanzo:*** *Data za uwandani (2022).*

Kiambishi-awali <ku-> kinapoambatishwa mwanzoni mwa mashina haya ya vitenzi yanayoanza kwa irabu, kuna mabadiliko kadhaa yanayotokea. Kwanza, umbo la irabu ya kiambishi-awali hubadilika kwani irabu hiyo huyeyushwa na kuwa kiyeyusho cha midomo. Pili, irabu ya kwanza ya shina la kitenzi, inayokabiliana na kiyeyusho hicho, hurefushwa ili kufidia urefu wa irabu iliyoyeyushwa. Na, tatu, idadi ya silabi za neno hupungua kwa silabi moja kwani kuyeyushwa kwa irabu ya kiambishi-awali hufanya kiambishi hicho kupoteza hadhi yake kama silabi inayojitegemea; badala yake, huungana na irabu ya kwanza ya shina la kitenzi ili kuunda silabi moja.

Hali ya vitenzi hivi (taz. Jedwali 3) kubadilika maumbo yake pindi vinapoambatishiwa kiambishi-awali <ku-> cha kitenzi kiso-ukomo inaelekea kuwa jambo linalotokea kwa nasibu tu. Mathalani, tunapochunguza matamshi ya vitenzi vingine vinavyotokana na shina la kitenzi <-enda> – kama vile <k**u**$^{w}$**e**ndea>, <k**u**$^{w}$**e**ndelea>, <k**u**$^{w}$**e**ndeleza>, <k**u**$^{w}$**e**ndesha> – tunaona kuwa irabu ya kiambishi-awali na ile ya kwanza katika shina la kitenzi hazibadiliki baada ya kufanywa kwa uambishaji. Ukiacha vitenzi hivi viwili tulivyovijadili hapa, kuna kitenzi kingine kimoja ambacho urefu wa irabu zake unaelekea kuathiriwa na uambishaji kisarufi kwa namna inayotofautiana kabisa na vitenzi vingine vyote vya Kiswahili sanifu, kama kinavyojadiliwa katika kipengele kinachofuata.

***Urefu wa irabu ya kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, kilichorithiwa kutoka Mame-Bantu, kwenye vitenzi vya Kiswahili sanifu***

Tunapozungumzia vitenzi vya Kiswahili sanifu kubadilika maumbo pindi mashina yake yanapoambatishiwa kiambishi-awali <ku-> ili kuunda kitenzi kiso-ukomo, kuna kitenzi kingine kimoja chenye tabia zisizofanana na vitenzi vingine tulivyovijadili katika vipengele vilivyopita.

Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/w8d1eq25


Kitenzi hicho ni kitenzi <kuja>. Kitenzi <kuja> hakielekei kuwa na shina linaloanza kwa irabu, bali konsonanti, <ku+**j**a>. Aidha, hiki ni kitenzi kimojawapo kati ya vitenzi kumi vya lugha hii vinavyotajwa kuwa na mzizi unaoundwa na silabi moja tu, kama vinavyoorodheshwa katika Jedwali 4.

*Jedwali 4: Vitenzi vya Kiswahili sanifu vyenye mizizi inayoundwa kwa silabi moja*

| **Na.** | **Kiambishi-awali** | + | **Mzizi** | + | **Irabu ishilizi** | → | **Kitenzi kiso-ukomo** | **Fasili** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | <ku | + | ch | + | a> | → | <kucha> | 'kuogopa, kuhofu' |
| 2 | <ku | + | ch | + | a> | → | <kucha> | 'kuchomoza kwa jua' |
| 3 | <ku | + | chw | + | a> | → | <kuchwa> | 'kuzama kwa jua' |
| 4 | <ku | + | nyw | + | a> | → | <kunywa> | 'kutia kimiminika kinywani na kukimeza' |
| 5 | <ku | + | ny | + | a> | → | <kunya> | 'kutoa haja kubwa' |
| 6 | <ku | + | w | + | a> | → | <kuwa> | 'kutokea, kutendeka, kufanyika' |
| 7 | <ku | + | l | + | a> | → | <kula> | 'kutia chakula kinywani na kukimeza' |
| 8 | <ku | + | p | + | a> | → | <kupa> | 'kukabidhi mtu kitu' |
| 9 | <ku | + | f | + | a> | → | <kufa> | 'kutokwa na uhai' |
| 10 | <ku | + | j | + | a> | → | <kuja> | 'kufika mahali fulani' |

***Chanzo:*** *Ashton (1977).*

Tunapochunguza kwa makini matamshi ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wanapotamka vitenzi hivi, tunaona wazi kuwa kitenzi <kuja> kina irabu ndefu katika kiambishi-awali kiso-ukomo, <ku->, ilhali vitenzi vingine vilivyobaki vina irabu fupi katika kiambishi-awali hicho.

Kana kwamba hiyo haitoshi, urefu huo wa irabu ya kiambishi-awali katika kitenzi <k**u:**ja> hauelekei kutokea kwenye umbo la kitenzi kiso-ukomo tu. Tunapochunguza maumbo ya maneno mengine yanayotokana na kitenzi <k**u:**ja>, tunabaini kuwa viambishi-awali vyake navyo vina irabu ndefu kabla ya mzizi wa maneno hayo, kama kilivyo kiambishi-awali cha kitenzi <k**u:**ja>. Hebu tulinganishe urefu wa irabu za viambishi-awali hivyo vya maneno yanayotokana na kitenzi <k**u:**ja> na ule wa irabu za viambishi-awali vya maneno mengine yasiyotokana na kitenzi <k**u:**ja>, katika Jedwali 5.

*Jedwali 5: Ulinganishi wa urefu wa irabu za viambishi-awali vya maneno yatokanayo na kitenzi <ku:ja> na wa irabu za viambishi-awali vya maneno yasiyotokana na kitenzi hicho*

| **Ngeli** | **Kiambishi** | **Neno linalotokana na kitenzi <ku:ja>** | **Fasili** | **Neno lisilotokana na kitenzi <ku:ja>** | **Fasili** |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | <wa-> | <**wa**jaji> | 'watu wanaokuja' | <**wa**juba> | 'wingi wa *mjuba*' |
| 4 | <mi-> | <**mi**jo> | 'namna za kuja' | <**mi**ji> | 'mahali pa nyumba nyingi' |
| 6 | <ma-> | <**ma**jilio> | 'kuja kwa jambo mara ya kwanza' | <**ma**kalio> | 'sehemu ya mwili ya kukalia' |
| 11/14 | <u-> | <**u**jaji> | 'namna ya kuja' | <**u**jaji> | 'kazi ya jaji' |
| | | <**u**jio> | 'tendo la kuja mtu maarufu au tukio maalumu' | <**u**jia> | 'uchochoro' |

***Chanzo:*** *Data za uwandani (2022).*

Uchunguzi wa matamshi ya maneno yaliyopo kwenye safu-mwimo ya kushoto, kama yalivyotamkwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu, unaonyesha kuwa viambishi-awali vyake husikika kuwa na irabu ndefu (<w**a:**ja:ji>, <m**i:**jo>, <m**a:**jilio>, <**u:**ja:ji>, <**u:**jio>); ilhali maneno yaliyopo kwenye safu-mwimo ya kulia yana viambishi-awali vyenye irabu zinazosikika kuwa fupi (<w**a**juba>, <m**i**ji>, <m**a**kalio>, <**u**ja:ji>, <**u**jia>).

Tunaweza kujiuliza: Je, ni kwa nini kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, katika kitenzi <k**u:**ja> cha Kiswahili sanifu husikika kikiwa na irabu ndefu, ilhali kiambishi-awali hichohicho katika vitenzi vingine hakisikiki kikiwa na irabu ndefu? Au, kwa kuongezea, ni kwa nini viambishi-awali vya maneno yaliyonyambuliwa kutokana na kitenzi <k**u:**ja> husikika vikiwa na irabu ndefu, ilhali viambishi-awali hivyohivyo vikiwa kwenye maneno yasiyotokana na kitenzi hicho vinasikika vikiwa na irabu fupi? Hebu ngoja tujadili hapa.

Kuwepo kwa irabu ndefu katika kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo kinachomaanisha 'kuja', na irabu ndefu katika viambishi-awali vya maneno mengine yanayotokana na kitenzi hicho, kunaelekea kuwa si jambo geni katika lugha fulani za Kibantu. Mathalani, katika ekiKwaya [EJ251] na eciRuuri [EJ253], lugha zinazozungumzwa mkoani Mara, kaskazini mwa Tanzania, kitenzi kinachomaanisha 'kuja' nacho kina irabu ndefu katika kiambishi-awali, <-*ku*->. Kana kwamba hiyo haitoshi, urefu huo wa irabu ya kiambishi-awali ndio pekee unaotofautisha maana ya kitenzi hicho na ile ya kitenzi kingine kinachomaanisha 'kwenda' katika lugha hizi. Jedwali 6 linafafanua.

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/w8d1eq25


*Jedwali 6: Tofauti ya urefu wa irabu ya kiambishi-awali cha kitenzi kinachomaanisha 'kuja' na kitenzi kingine katika ekiKwaya na eciRuuri*

| **Kiambishi-awali-kitangulizi** | + | **Kiambishi-awali** | + | **Mzizi** | + | **Irabu ishilizi** | → | **Kitenzi kiso-ukomo** | **Fasili** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *<o-* | + | *-**ku**-* | + | *-j-* | + | *-a>* | → | *<o**ku**ja>* | 'kwenda' |
| *<o-* | + | *-**ku:**-* | + | *-j-* | + | *-a>* | → | *<o**ku:**ja>* | 'kuja' |

***Chanzo:*** *Kiraka & Roth (2007); Massamba (2005b).*

Jedwali hili linaonyesha kuwa katika ekiKwaya [EJ251] na eciRuuri [EJ253], kitenzi <*okuja*> 'kwenda' kina irabu fupi, <*-u-*>, inayotokea kwenye kiambishi-awali kiso-ukomo, kabla ya mzizi wa kitenzi. Kwa upande mwingine, kitenzi <*oku:ja*> 'kuja' kina irabu ndefu, <*-u:-*>, inayotokea kwenye kiambishi-awali kiso-ukomo, kabla ya mzizi wa kitenzi, kama ilivyo kwa kitenzi <k**u:**ja> katika Kiswahili sanifu! Hivyo basi, kuwepo kwa irabu ndefu kwenye kiambishi-awali cha kitenzi kinachomaanisha 'kuja' si jambo geni, wala la ajabu, katika baadhi ya lugha za Kibantu.

Jambo la kuvutia zaidi kuhusu kitenzi <k**u:**ja> katika Kiswahili sanifu ni kwamba baadhi ya maneno yanayotokana na kitenzi hicho yana kiambishi-awali kinachoundwa kwa konsonanti pekee, bila irabu yoyote, kinachotokea kabla ya mzizi wa maneno hayo, kama zilivyo irabu ndefu za viambishi katika maneno mengine yanayotokana na kitenzi <k**u:**ja>! Kwa hiyo, tunaweza kujiuliza: Je, konsonanti hiyo inayotokea kabla ya mzizi wa maneno hayo nayo inaweza kusikika ikiwa ndefu? Hebu tulinganishe urefu wa kiambishi-awali <m-> cha nomino zinazotokana na kitenzi < k**u:**ja> na ule wa kiambishi-awali <m-> cha nomino zisizotokana na kitenzi <k**u:**ja>, katika Jedwali 7.

*Jedwali 7: Ulinganishi wa urefu wa konsonanti za viambishi-awali vya nomino zinazotokana na kitenzi <ku:ja> na wa konsonanti za viambishi-awali vya nomino zisizotokana na kitenzi hicho*

| **Ngeli** | **Kiambishi-ngeli** | **Nomino kutoka kitenzi <ku:ja>** | **Fasili** | **Nomino nyinginezo** | **Fasili** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | <m-> | <**m**jaji> | 'mtu anayekuja' | <**m**juba> | 'mtu fidhuli na jeuri' |
| 3 | <m-> | <**m**jo> | 'namna ya kuja' | <**m**ja> | 'mtu, binadamu' |
| | | <**m**jio> | 'sababu ya kuja' | <**m**jao> | 'hali ya kujaa' |

***Chanzo:*** *Data za uwandani (2022).*

Uchunguzi wa matamshi ya wazungumzaji ya nomino zilizopo kwenye safu-mwimo ya kushoto, zinazotokana na kitenzi <k**u:**ja>, unaonyesha kuwa viambishi-awali vyake husikika kuwa na konsonanti ndefu (<**m:**ja:ji>, <**m:**jo>, <**m:**jio>); ilhali nomino zilizopo kwenye safu-mwimo ya kulia, zisizotokana na kitenzi <k**u:**ja>, zina konsonanti za viambishi-awali zinazosikika kuwa fupi (<**m**juba>, <**m**ja>, <**m**jao>). Hali hii ya viambishi-awali vya nomino hizi – ambavyo huundwa kwa konsonanti pekee – kusikika vikitamkwa kwa wakaa mrefu, ilhali viambishi-awali vingine vikitamkwa kwa wakaa mfupi, inadokeza kuwa baadhi ya konsonanti za Kiswahili sanifu zinaweza

pia kuwa fupi au ndefu, kama zilivyo irabu za lugha hii. Kuwepo kwa konsonanti fupi na konsonanti ndefu nalo si jambo geni, wala la ajabu, katika lugha za Kibantu kwani baadhi ya lugha hizo, kama vile Luganda [EJ15], hutajwa kuwa na konsonanti fupi na konsonanti ndefu (taz. Hyman, 2014; Katamba, 1993).

Sifa hizi zinazohusu nyakaa za baadhi ya konsonanti zinazounda baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu yanayotokana na kitenzi <ku:ja> ni sifa za kusisimua katika duru za isimu ya lugha hii ya Kibantu! Kwa kuwa utafiti huu ulikusudiwa kuchunguza sifa zinazohusu urefu wa irabu katika maneno fulani ya Kiswahili sanifu, na si katika konsonanti zake, hatutazizamia sifa za urefu wa konsonanti katika maneno ya lugha hii. Mada hiyo inaweza kuchunguzwa kwa utafiti mwingine. Kwa sasa, tuendelee kuchunguza sababu za kutokea kwa irabu hiyo ndefu katika kiambishi-awali cha kitenzi <k**u:**ja>.

***Sababu za kutokea irabu ndefu kwenye kitenzi <ku:ja> katika Kiswahili sanifu na lugha nyingine za Kibantu***

Kama tulivyodokeza awali, tunaweza kujiuliza: Je, ni kwa nini kitenzi <k**u:**ja>, au kitenzi kinachomaanisha 'kuja', na maneno mengine yanayotokana na kitenzi hicho, katika Kiswahili sanifu na baadhi ya lugha za Kibantu, husikika kuwa na irabu ndefu kwenye kiambishi-awali kinachopakana na mzizi wa neno? Katika kujaribu kujibu swali hili, utafiti huu ulichunguza maumbo ya neno linalomaanisha 'kuja' yaliyoundilizwa katika lugha ya Mame-Bantu, lugha iliyozaa Kiswahili sanifu na lugha nyingine za Kibantu. Tulifanya hivyo ili kuona kama kuna kufanana kokote kwa maumbo ya neno hilo baina ya lugha hiyo ya kale na lugha za sasa zilizorithi msamiati wake mwingi kutoka lugha hiyo. Hali kadhalika, tulizingatia kuwa kitenzi <ku:ja> ni sehemu ya msamiati msingi wa lugha, msamiati unaotajwa kuwa na tabia ya kutobadilikabadilika sana katika lugha (Massamba, 2007). Jedwali 8 linaonyesha mzizi na shina la kitenzi kinachomaanisha 'kuja' katika lugha ya Mame-Bantu kutoka tafiti mbili tofauti zilizoundiliza maumbo ya baadhi ya maneno ya lugha hiyo ya kale.

*Jedwali 8: Mzizi / shina la neno linalomaanisha 'kuja' katika Mame-Bantu*

| Chanzo | Mzizi / shina la kitenzi | Fasili |
|---|---|---|
| **Nurse & Philippson (1975):** | **-yij-* | 'mzizi wa kitenzi kinachomaanisha "kuja" katika Mame-Bantu' |
| **Bastin, Coupez & Mann (1999):** | **=jij-a* | 'shina la kitenzi kinachomaanisha "kuja" katika Mame-Bantu' |

***Chanzo:*** *Nurse & Philippson (1975); Schadeberg (2014).*

Taarifa za uundilizaji wa maneno ya lugha ya Mame-Bantu zilizopo katika Jedwali 8 zinaonyesha kuwa mzizi wa kitenzi kinachomaanisha 'kuja' katika lugha ya Mame-Bantu ulikuwa na silabi mbili, <**-yi-*> na <**-j-*>, au <**=ji-*> na <**-j-*>. Kwa upande mwingine, tumeona hapo awali kuwa mzizi wa kitenzi kinachomaanisha 'kuja' katika baadhi ya lugha za sasa za Kibantu unaundwa kwa silabi moja tu, <-j-> (taz. Jedwali 4 na Jedwali 6). Silabi hii ya mzizi wa kitenzi 'kuja' katika baadhi ya lugha za sasa za Kibantu, <-j->, inafanana na silabi ya pili ya mzizi wa kitenzi hicho katika lugha ya Mame-Bantu, <**-j-*>. Silabi ya kwanza ya mzizi wa kitenzi hicho katika lugha ya Mame-Bantu, <**-yi-*> au <**-ji-*>, haielekei kuwakilishwa katika mzizi wa kitenzi hicho katika baadhi ya lugha za sasa za Kibantu, kama vile Kiswahili sanifu na baadhi ya lugha za Kibantu za eneo la Maziwa Makuu tulizozirejelea hapo awali. Kwa sababu hiyo, tunaweza kufupisha mjadala huu kwa kusema kuwa

baadhi ya lugha za sasa za Kibantu, kama vile Kiswahili sanifu, huelekea kurefusha irabu au konsonanti inayotokea kabla ya mzizi wa kitenzi <ku:ja>, au kabla ya mzizi wa maneno yanayotokana na kitenzi hicho, ili kufidia silabi ya kwanza ya mzizi wa kitenzi hicho iliyokuwepo katika lugha ya Mame-Bantu, silabi ambayo ilidondoshwa na lugha za sasa za Kibantu.

**Hitimisho**

Makala hii imewasilisha matokeo ya utafiti uliochunguza iwapo kiambishi-awali cha kitenzi kiso-ukomo, <ku->, kinaweza kuathiri urefu wa irabu kinapoambatishwa kwenye maumbo ya utenda ya vitenzi vya Kiswahili sanifu. Matokeo ya uchunguzi yameonyesha kuwa kiambishi-awali hicho kinaweza kuathiri urefu wa irabu za maumbo mapya ya vitenzi yanayozaliwa kulingana na aina ya vipashio vinavyotokea mwanzoni mwa shina la utenda la kitenzi husika, yaani kama ni irabu au konsonanti, au kulingana na sifa za kitenzi zilizorithiwa kutoka lugha ya Mame-Bantu.

**Marejeleo**

Ashton, E. O. (1977). *Swahili grammar (including intonation)* (3rd impression). Longman Group Ltd.

Baraza la Kiswahili la Taifa (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili* (Chapa ya 3). Longhorn Publishers Limited.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2015). *Kamusi la Kiswahili fasaha* (Chapa ya 2). Oxford University Press.

Choge, S. C. (2009). Understanding Kiswahili vowels. *The Journal of Pan African Studies, 2*(8), 62–77.

Crystal, D. (2008). *A dictionary of linguistics and phonetics* (6th ed.). Blackwell Publishing.

Hyman, L. M. (2014). Basaá (A43). In D. Nurse & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (pp. 257–282). Routledge.

Ismail, J. H. (2025). The impact of compensatory vowel lengthening in phonological processes among Standard Kiswahili words. *SAUT Multidisciplinary Journal of Education, 4*(1).

Katamba, F. (1993). *Morphology*. St. Martin's Press.

Kimizi, M. M. (2003). *The syllable structure in standard Kiswahili* [Unpublished masters dissertation]. University of Dar es Salaam.

Kiraka, P. (2025). Toni inavyoathiri urefu wa irabu za viambishi-awali vya nomino za Kiswahili. *Nuru ya Kiswahili, 4*(2).

Kiraka, P. (2023). Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu katika Kiswahili Sanifu. *Nuru ya Kiswahili, 2*(1), 27–48.

Kiraka, P. (2013). *Urefu, urefushaji na ufupishaji wa irabu katika Kiswahili sanifu* [Tasnifu ya shahada ya umahiri ambayo haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiraka, P. & Roth, T. (2007). *Kwaya orthography sketch: Internal report*. SIL International.

Maganga, C. (1991). *A study of the morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi* [Unpublished doctoral thesis]. University of Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (2005a). The role of 'suprasegmental' phenomena in the analysis of Bantu languages: With special reference to Ciruuri. *Occasional Papers in Linguistics*, 1, 88-105.

Massamba, D. P. B. (2005b). *Kamusi ya ciRuuri-Kiswahili-Kiingereza*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili origins and the Bantu divergence-convergence theory*. Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nandelenga, H. S. (2022). Phonological processes in the acquisition of Kiswahili: An Optimality

Theory perspective. *Journal of Literature, Languages and Linguistics, 85*, 12–25. https://doi.org/10.7176/JLLL/85-03
Ndumiwe, E. J. (2021). Athari za irabundefu kwenye maana na uainishaji wa maneno yenye jozi pambanuzi finyu katika lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2013). *Kioo cha Lugha, 19*(2), 123–136.
Nurse, D., & Philippson, G. (1975). *Tanzania language survey data* [Unpublished wordlists].
Schadeberg, T. C. (2014). Derivation. In D. Nurse & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (pp. 71–120). Routledge.
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la tatu). Oxford University Press.
Trask, R. L. (1996). *A dictionary of phonetics and phonology*. Routledge.